

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam
Tarehe 16 Juni 2007**

Mahudhurio

Ally Salum

Elaine Baker

Juma Ali Salehe Jongo

Kibwana Mohammad Msiga

Rashidi Saidi Karanji

Sosthenes C Amlima

Mawasiliano na Manispaa ya Ilala

Sosthenes alarifu kuwa yeye, Mejah, Posper na Juma walihudhuria kikao cha idara ya usariri pamoja na manispaa ya ilala tarehe 15 Mei. Mejah na prosper walitoa mada kwa pamoja na kugawa picha. Sehemu kubwa ya mjadala ilijikita zaidi kwenye daladala na kulikuwa na mapendekezo kwamba kuwe na kampuni moja moja za kudhibiti safari husika za daladala amabazo zingeingia mkataba na wenye mabasi. Kikao kiliteua nguvu kazi itakayoendelea kujadili suala la msongamano. Prosper aliteuliwa kwenye nguvu kazi hii. Elaine alisema aliongea na prosper kwa simu na kusema kuwa mpaka sasa hakuna kikao kilichofanywa na nguvu kazi hiyo.

Alihamisi iliyopita tarehe 14 Juni, gazeti la citizeni liliandika katika ukurasa wake wa kwanza na wa pili, makala iliyosema kwamba manispaa ya ilala ilipiga marufuku mafuta na mikokoteni kufika katikati ya jiji. Elaine alishangazwa na hilo kwa sababu manispaa ya Ilala siku chache kabla ilimhakikishia kwamba sera hiyo isingendelea. Elaine alitembelea ofisi ya meya wa ilala Ijumaa na Meya alimwambia kuwa makala ile haikuwa sahihi na hakukuwa na kizuizi chochote cha maguta na mikokoteni kuingia katikati ya jiji. Elaine alipiga simu kwa gazeti la The Citizen na kuongea na mwandishi wa makala ile na kukiri kwamba haikuwa sahihi.

Barabara zilizopangwa kujengwa

Juama aliarifu kuwa alikwenda kwa wakala wa Barabara kutafuta mawasiliano na mahali zilipo ofisi za wataalamu – washauri na wakandarasi wanaohusika na barabara tatu – sam Nujoma, Nelson Mandela na Kilwa. Elaine aliandika barua iliyolenga kutafakari suala tulilokuwa nalo katika kikao kilichopita Barua hii itakwenda kwa wataalamu – washauri, wakandarasi, wakala wa Barabara dar es Salaam na makao makuu. Watu wengine kwenye kikao waliangalia barua na kufanya masahihisho.

Msafara wa Baiskeli

Hatua ya kwanza ya mapendekezo yetu ya msafara wa baiskeli ni kupata ufadhili. Elaine aliandika barua kuomba ufadhili na wanachama wengine walifanya masahihisho. Tulitafakari orodha ya makampuni tutakayoomba ufadhili na kuyagawa katika makundi.

Mjini na kariakoo

- Azam (Said Salumu Bakresa) – Ofisi zao Bandarini Kurasini
- Vodacom – Ofisi zao mtaa wa Ohio
- Tigo – Ofisi kariakoo
- National Microfinance Bank.
- Bank ya tatifa ya biashara (NBC) Ubalonzi wa Uholanzi

Mwenge na Maeneo ya Jirani

- IPP (BW. Mengi) – Mwenge
- Celtel – Kijitonyama
- NABICO – Mwenge

Barabara ya Nyerere

- Mohammed Enterprises – Barabara ya Nyerere
- Knight Support – Karibu na TAZARA
- Kampuni ya Mafuta – Barabara ya Nyerere

Wengine

- Zantel – ofisi karibu na ubalozi wa Marekani

Kwa kila kampuni tutapeleka barua ya kiingereza na Kiswahili, nakala ya mapendekezo na nakala ya cheti cha usajili wa shirika letu la kiserikali (NGO)

Mengineyo

Sosthenes aliarifu kwamba alikuwa Mlimani city na hawazui tena baiskeli kuingia au kuegesha . lakini , bado hapajawekwa nyenzo au vifaa maalum kwa ajili ya maegesho ya baiskel. Kulikuwa pia na mjadala juu ya kupata ofisi. Kikwazo ni pesa – kuwa na ofisi itahitaji kodi ya pango kila mwezi na mshahara wa kila mwezi kwa ajili ya mtu atakae kuwa anakaa ofisini, ambaye atahitaji kama Tsh. 100,00/= kwa mwezi. Ni vigumu kupata wafadhili wa kudumu. Eneo la ukumbi wa kikao ulijadiliwa. Ilipendekezwa kwamba tukutane Mabibo – Mahakama ya Ndizi kwa kuwa kuna maguta mengi na baiskeli za kukodi katika eneo hilo. Ilikubalika tukutane ofisini kwa Jumanne ambapo maguta hutengenezwa. Ni karibu na maktaba Baa. Ilikubalika kwamba Rashid afuatilie ili ikikubalika amtaarifu Elaine kasha Elaine atawatumia umumbe wamumbe kuhusu eneo la kikao cha wiki ijayo.